



سمندری گنبد

Kuba Baharini

(Swahili)



SHEIKH-E-TARIQAT AMEER-E-AHLESUNNAT MUANZILISHI WA
DAWAT-E-ISLAMI HAZRAT ALLAMAH MAULANA ABU BILAL
MUHAMMAD ILYAS ATTAR QADIRI RAZAVI رحمۃ اللہ علیہ

Imetolewa na: Majlis-e-Tarajim
(Dawat-e-Islami)

سَمندری گنبد

Kuba Baharini

(Haki za Wazazi katika Uislamu)

Kijitabu hiki kiliandikwa na Shaykh-e-Tariqat Amīr-e-Ahl-e-Sunnat, muanzilishi wa Dawat-e-Islami 'Allāmah Maulānā Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qadiri Razavi دامت برکاتہم العالیہ

Katika lugha ya Kiurdu. Kimetafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili na Majlise Tarajim. Endapo utaona makosa yoyote katika tafsiri yake au utungaji wake, tafadhali wajulishe Majlise Tarajim kwa njia ya posta au kwa kipepesi ili upate thawabu.

Majlise Tarajim (Dawat-e-Islami)

Alami Madani Markaz, Faizan-e-Madina, Mahalla Saudagran,
Old Sabzi Mandi, Baab-ul-Madina, Karachi, Pakistan
Wasiliana kwa nambari: +92-21-34921389 hadi 91
translation@dawateislami.net

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ط

Dua Kabla Ya Kusoma Kitabu

Kabla ya kusoma kitabu au somo la kidini, soma dua ifuatayo.
Insha-Allah عَزَّوَجَلَّ utakumbuka yote uliyoyasoma.

اللَّهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَاذْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَا الْجَلَالِ وَالْإِكْرَامِ

Ee mola عَزَّوَجَلَّ Ifungue milango ya elimu na busara kwa ajili yetu, na utuhurumie! Ewe ulie mtakatifu kabisa.

(Al-Mustatraf Vol. I, P. 40, Dar-ul-Fikr, Beirut)

Kumbuka: Mswalie Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ mara moja kabla na baada ya dua.

(Roohani Hikiyyat UK. 68)

الْحَمْدُ لِلَّهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ وَالصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ عَلَى سَيِّدِ الْمُرْسَلِينَ
أَمَّا بَعْدُ فَأَعُوذُ بِاللَّهِ مِنَ الشَّيْطَانِ الرَّجِيمِ بِسْمِ اللَّهِ الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ ط

Kuba Baharini



Shetani atatumia kila hila ili kukuzuia kusoma kitabu hiki, lakini utaingiwa na hofu ya Allah عَزَّوَجَلَّ kubwa baada ya kukisoma *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ*.

Aliyemsalia Mtume ﷺ Kwa Sauti Alisamehewa

Mzee mmoja mcha Mungu alimuona mtu aliyekufa katika ndoto na akamuuliza, “Je Mola عَزَّوَجَلَّ amekuhukumu vipi wewe? Yule aliyekuwa amekufa akajibu, “Mola عَزَّوَجَلَّ amenisamehe.” Yule mcha Mungu akauliza, “Kwa sababu gani?” Akajibu, “Nilikuwa nikimuandikia Muhaddith hadithi. Wakati mmoja akamsalia Mtume, mwenye nur, rehma ya dunia zote mbili, kipenzi cha Allah صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa hivyo nami nikamsalimia mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwa sauti. Kila aliyenisikia, naye pia akamsalia mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. Kwa hivyo kutokana na hilo Allah عَزَّوَجَلَّ akatusamehe sote.”

(Al-Qaul-ul-badi uk. 204)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Allah عَزَّوَجَلَّ alimteremshia wahyi Sayyiduna Sulayman عَلَى تَبِيئَتَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ akimuamrisha kutembelea ufuo wa bahari ili kushuhudia nguvu za uwezo wake. Sayyiduna Sulayman عَلَى تَبِيئَتَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ alienda na wafuasi wake lakini hakuona kitu chochote (cha maajabu). Kwa hivyo aliamuamrisha jinni kupiga mbizi baharini ili amletee habari za ndani. Baada ya kutoka mle baharini, yule jinni alisema, “Sikuweza kufikia kina cha bahari na wala sikuona kitu chochote cha kueleweka.” Akamuamrisha jinni mwingine ambaye alikuwa na nguvu zaidi ya yule wa kwanza. Jinni huyu wa pili alienda mbizi mara mbili ya kina cha yule wa kwanza lakini hata yeye hakuweza kuleta habari yoyote. Baadaye akamuamrisha waziri wake mwenye busara, Waziri Shaykh Asif bin Barkhiya رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ.

Kwa muda mfupi sana, Asif Barkhiya رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alileta kuba kubwa jeupe la kafuri lenye milango minne mbele ya mahakama ya Sayyiduna Sulayman (عَلَى تَبِيئَتَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ). Mlango mmoja ulikuwa umetengenezwa kwa lulu, wa pili kwa yakuti, wa tatu kwa almasi na wa nne kwa zumaridi. Kuba lenyewe halikuwa na tone moja la maji ijapokuwa milango yote ilikuwa wazi. Ndani ya kuba hili kulikuwa na kijana mwenye umbile zuri, aliyevalia nguo safi na maridadi akiwa katika sala. Alipomaliza kuswali, Sulayman (عَلَى تَبِيئَتَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ) akamsalimia na akataka kujua kuhusu siri ya kuba lile. Akasema: “Ewe Mtume wa Mwenyezimungu اِحْسَنَ اللهُ تَعَالَى عَلَيَّوْ وَالِهٖ وَسَلَّم. Baba yangu alikuwa mlemavu na mama yangu alikuwa kipofu عَزَّوَجَلَّ. Niliwatumikia kwa miaka sabini. Kabla ya mamangu kufariki aliomba ya kwamba:

“Ewe Mwenyezimungu **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ** nakuomba umjaalie mwanangu umri mrefu wa heri.” Babangu kipenzi kabla ya kufariki naye pia aliomba: “Ewe Mwenyezimungu **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** nakuomba umjaalie uwezo mwanangu wa kuabudu mahali ambapo shetani hataweza kumghilibu.”

Baada ya kumzika babangu nilikuja katika ufuo huu nikalionga kuba hili nikaingia ndani. Wakati huo huo alikuja malaika na akalipeleka kuba hili mwisho wa kina cha bahari.” Alipoulizwa na Sayyiduna Sulayman **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَام** kuhusu muda alioishi mule. Alijibu, “Nimeishi hapa tangu enzi ya nabii Ibrahim **عَلَيْهِ السَّلَام**.” Sulayman **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَام** alitambua kuwa imempita miaka elfu mbili tangu aingie katika kuba lile na bado angali kijana na hata hakuwa na unywele mmoja mweupe katika kichwa chake!

Alipoulizia kuhusu chakula chake alisema: Kila siku ndege wa rangi ya kijani kibichi huniletea kitu cha rangi ya manjano mdomoni mwake nami hukila. Kina ladha ya utamu wote wa duniani. Kinanitosheliza kwa njaa na kiu. Juu ya hayo **اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ عَزَّوَجَلَّ**, nimesalimika na joto, baridi, usingizi, uvivu, upweke, uwoga na vituko. Baada ya hapo, kutokana na ombi la yule kijana na kuamrisha na Sulayman **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَام** Shaykh Asif bin Barkhiya **رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ** ali lichukuwa kuba na akalirudisha ndani ya bahari.

Baada ya haya Sulayman **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَام** alisema: “Enyi watu, Mwenyezimungu **صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ** awateremshie rehema zake.

Je, mumeona jinsi maombi ya wazazi yanavyotakabaliwa! Jiepusheni na kuwakosea wazazi wenu.” (*Raud-ur-Riyahin, uk. 233*)

Rehma Za Mwenyezimungu Ziwashukie Na Tupate Msamaha Kwa Baraka Zao.

Ndugu wapendwa waislamu! Tumefahamu ya kwamba, kuwatumikia wazazi ni sudi kubwa. Wanapofurahi na kutuombea, tunafaulu. Sikiliza kisa kingine cha kuzidisha imani na kitakachokujaza furaha.

Kidole Kilichoumia

Sayyidina Bayazid Bistami رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema: Mamangu alinituma maji katika usiku wa baridi kali katika majira ya baridi. Nilimpelekea glasi ya maji lakini alikuwa ameshalala. Sikuona sawa kumuamsha kwa hivyo nilisimama karibu naye na glasi ya maji nikimngojea aamke. Kwa kuwa nilisimama kwa muda mrefu, maji yalitiririka mikononi mwangu na yakageuka kuwa barafu.

Mamangu alipoamka, nilimkabidhi ile glasi ya maji. Baada tu ya kidole kilichokuwa kimeshikana na glasi kilipoachana, ngozi ikabanduka na kikaanza kutoa damu. Baada ya kuona haya, mamangu aliniuliza: “Kidole kina nini?” Nikamsimulia kisa chote. Halafu akanyanyua mikono yake na akaomba: Ewe Mwenyezimungu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ nimeridhika naye, nakuomba pia nawe uwe radhi naye. (*Nuzha-tul-majalis, pp.261, v.1*) Rehma za

Mwenyezimungu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ ziwashukie na tupate msamaha kwa baraka zao.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Busu Kizingiti Cha Mlango Wa Pepo Kila Siku.

Waliobahatika, ni wale ambao wazazi wao wangali hai, wanastahili kuwabusu miguu na mikono yao angalau mara moja kwa siku. Kuna thawabu kubwa kwa kuwaheshimu wazazi. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: *الْجَنَّةُ تَحْتَ أَقْدَامِ الْأُمَّهَاتِ* “Pepo iko chini ya nyayo za mama.” Yaani ukiwatendea mazuri malipo yake ni pepo. Imeandikwa katika Bahar-e-shariat, juzu 16, ukurasa 88 iliyochapishwa na Maktabatul-Madinah: Mtu anaweza pia kubusu miguu ya mamake. Imeandikwa katika hadithi “Mwenye kubusu miguu ya mamake ni kama aliyebusu kizingiti cha peponi.”

(Dur-ru-Mukhtar, p. 606 v. 9)

Aliwaacha Huru Watumwa Wawili Kwa Sababu Ya Kunyanyua Sauti Mbele Ya Mama

Wakati wowote unapomuona mamako au babako anakuja, simama kwa heshima. Usizungumze nao kwa kuwalenga macho yao. Pindi wanapokuita, bila ya kuchelewa, itikia “Labbaika” (niko hapa). Zungumza nao kwa unyenyekevu (na usienue sauti yako juu ya yao). Sayyiduna Abdullah bin Awn aliitwa na mama yake na alipoitika, sauti yake kidogo ilikuwa juu. Kwa sababu

hiyo alilipa fidia kwa kuwaachilia huru watumwa wawili.
(*Hilyat-ul- Awliya, uk. 45, Juzuu 3 Raqam 3103*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Pata Thawabu Ya Hijja Yenye Kutakabaliwa

رَحْمَتُهُمُ اللهُ الْعَزِيزِ (Tazama) namna gani wacha Mungu walivyowathamini wazazi wao na namna fikra zao (za madani) za hali ya juu zilivyokuwa. (Huenda mtu akafikiria) Tutawatowa wapi watumwa wawili! Hatuwezi! Katika hali kama hiyo, sahu habari ya kuku wawili, hatuna hata ujasiri wa kutoa sadaka ya mayai mawili kwa ajili ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Mungu عَزَّوَجَلَّ atujaaliye tuujue umuhimu wa wazazi. Amin!

Acha tupate malipo makubwa bila ya kutumia chochote na kwa bure kabisa. Waangalie wazazi wako kwa huruma na mapenzi. Ni vizuri ulioje kuwaangalia wazazi wako kwa jicho la huruma! Mtume wa Mwenyezimungu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema: Watoto wakiwaangalia wazazi wao kwa jicho la huruma, Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ huandika thawabu ya Hijja yenye kukubaliwa kwa kila watakapowaangalia. Maswahaba watukufu عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانِ wakauliza: Hata kama mtu atawaangalia mara mia moja kwa siku! Mtume akasema, نَعَمْ، اللهُ أَكْبَرُ وَأَطْيَبُ “Ndiyo, Allah عَزَّوَجَلَّ ndiye mkubwa kabisa na aliyetakasika.” (*Shiab-ul-Iman, uk.186, Juzuu 6, Hsadih 8756*)

Bila ya shaka, Allah عَزَّوَجَلَّ ni muweza wa kila kitu. Anaweza عَزَّوَجَلَّ kutoa kingi anavyotaka. Hajawekewa mipaka au kulazimishwa

na yeyote, kwa hivyo iwapo mtu atawaangalia wazazi wake kwa njia ya huruma mara mia moja kwa siku, yeye **عَزَّوَجَلَّ** atamtuza zawadi ya Hijja mia moja zilizotabaliwa

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Rafiki Wa Peponi

Wakati mmoja Sayyiduna Musa **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ** alimuuliza Allah **عَزَّوَجَلَّ** “Ewe Mola msamehevu mno! Nionyeshe rafiki yangu wa peponi? Allah **عَزَّوَجَلَّ** akasema: Nenda mji fulani. Utamuona mchinjaji fulani ambaye ndiye atakayekuwa rafiki yako wa peponi. Kwa hivyo, Sayyiduna Musa **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ** alienda kwa mchinjaji. (Hata kama hakumtambua, alimkaribisha Sayyiduna Musa **عَلَيْهِ السَّلَامُ** kama msafiri na mgeni). Walipokaa wote pamoja kula, aliweka kapu kubwa karibu naye. Kila alipokula, alimenya tonge mbili akatia kapuni, halafu akamenya tonge moja akala yeye mwenyewe. Mara mtu mmoja akabisha mlango. Mchinjaji akasimama na akatoka nje. Sayyiduna Musa **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ** akaangalia kapuni, akawaona vikongwe wawili mke na mume wakiwa ndani. Punde tu walipomwaangalia Sayyiduna Musa **عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ**, walitabasamu. Walimtolea ushuhuda Sayyiduna Musa kuhusu utume wake. Na wakati huo huo tu wakafariki.

Mchinjanji aliporudi na kuwatazama wazazi wake wawili walikuwa wamefariki ndani ya kikapu, aliifahamu habari yote na akaibusu

mikono miwili ya Sayyiduna Musa عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ na akasema: Unaonekana kuwa wewe u Mtume wa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ Musa عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ akauliza: Umenijuaje? Akasema: wazazi wangu walikuwa wakiomba kwa unyenyekevu kila siku: “Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ Usitufishe mpaka tutakapomwona Sayyiduna Musa عَلَيْهِ السَّلَامُ. Kutokana na kifo chao, ndiyo nimekutambua kwamba wewe ndiye Musa عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ.”

Mchinjaji aliendelea kusema: Kila mamangu alipomaliza kula, alikuwa akiniombea kwa furaha kwa kusema: Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ mfanye mwanangu awe rafiki wa Musa عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ katika pepo. Musa عَلَى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ akasema: Pongezi! Allah عَزَّوَجَلَّ amekufanya kuwa rafiki yangu wa peponi. (*Nuzha-tul-Majalis, uk. 226, Juzuu.1*)

Rehma Za Mwenyemungu عَزَّوَجَلَّ Ziwashukie Na Tupate Msamaha Kwa Baraka Zao.

Adhabu ya kutotwii wazazi huanzia katika maisha ya hapa duniani Ndugu wapendwa waislamu! Je, mumeona? Ni namna gani dua za wazazi kuwaombea watoto wao zinavyotakabaliwa! Iwapo wazazi watakasirika na kuwaapiza watoto wao, maapizo hayo pia yatatakabaliwa. (Kwa hivyo) inapasa wazazi wafurahishwe wakati wote. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema:

“Wazazi ndiyo moto wenu na pepo yenu.” Katika hadithi nyingine Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema: Allah عَزَّوَجَلَّ akitaka anaweza kuchelewesha adhabu kwa kila dhambi hadi siku ya Hisabu

(kiyama) lakini adhabu ya mwenye kuwakosea wazazi wawili humpa hapa hapa duniani. (*Al- Mustadrak, uk. 216, Juzuu. 5 Hadith 7345*)

Mtu Mmoja Anakuwa Bubu Kwa Kukosa Kumuitikia Mamake

Imesimuliwa ya kwamba mtu mmoja alikosa kuitika alipoitwa na mamake. Kwa sababu hii mamake akamuapiza na akawa bubu. (*Bir-rul-Walidain lit-Tartushi, uk. 79*)

Ni Bora Wazazi Kujizuia Kuapiza (Watoto)

Ndugu Waislamu wapendwa! Mumeona! Yule ambaye hakumuitikia mamake alikuwa bubu papo hapo! Kuna mazingatio kwa wanaowakosea wazazi, hata hivyo kuna wakati wazazi nao pia wanastahili kufikiria. Hususan wale kina mama ambao huwaapiza watoto kwa kusema: Mola akuangamize, akujaalie ushikwe na ukoma n.k. Inaweza kuwa ni wakati wa maombi kutakabaliwa, na endapo apizo hilo litakubaliwa, kitu kibaya huenda kikamkumba mtoto huyo. Mama naye huenda akadhikika kwa yale yaliyompata mwanawe. Kwa hivyo ni vizuri wakati wote mama kuwaombea mema watoto wake.

Itabidi Kuregea Hata Kama Uko Ng'ambo.

Bila ya shaka, ni sudi kubwa kusafiri na Madani Qafila wa Dawat-e-islami pamoja na wapenzi wa Mtume ili kujifunza Sunnah. Pia ni sudi kubwa kusafiri katika Madani Qafilah ya Dawa-e-

Islami na kusambaza kazi za Madani, kusafiri nchi za ng'ambo na kukaa huko kwa miezi 12 au 25 lakini endapo wazazi watakukasirikia kutokana na hili au watapata shida sana kwa wewe kufanya hivyo, basi usisafiri. Lengo hasa la kueneza Dawat-e-Islami ulimwenguni si kupata sifa za mtu binafsi bali ni kumridhisha Allah عَزَّوَجَلَّ na kumridhisha Allah عَزَّوَجَلَّ hakuwezi kupatikana kwa kuwaudhi wazazi.

La ziada ni kwa wale wanaofanya kazi au biashara katika miji au nchi nyingine, ni lazima watii wazazi wao wanaposafiri. Liweke hili akilini kwani limeandikwa katika **Bahar-e-Shariat**, Juzuu 16 ukurasa wa 202 kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah: Mtoto akiwa ng'ambo na wazazi wamwite ni lazima arudi kwao. Kuwaandikia barua tu hakutoshi. Na pia iwapo wazazi watamuhitaji awatumikie, ni lazima arudi awatumikie.

Mtoto Mchanga Aongea!

Wakati wowote wazazi wakikuita, usichelewe kuitikia bila ya sababu. Watu wengine hupuuzwa sana jambo hili. Allah عَزَّوَجَلَّ atulinde; (watu wengine) hata hawaoni kwamba kuchelewa kuitikia ni makosa. Iwapo mtu ataswali swala ya sunna bila ya wazazi kujua halafu wamwite, itambidi avunje swala na awaitikie. (hata hivyo ni wajibu kuirudia swala ile baadaye).

Wale wanaowaudhi wazazi wao kwa kuwapuuzwa wanapowaita bila ya sababu wanapata madhambi makubwa na wanastahili kwenda motoni. Iwe iwayyo, mama ni mama. Wakati mwengine kwa kuchanganyikiwa, neno baya humtoka kinywani dhidi ya

mtoto wake. Endapo litatakabaliwa, mtoto atakuwa mashakani. Kulingana na jambo hili, hadithi nzuri ya maadili ya mcha Mungu kutoka Bani Israil imeelezwa katika Bukhari Sharif.

Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: Kulikuwa na mtu ajulikanaye kama Juraij katika Bani Israil. Alipokuwa akiswali, mamake alimwita lakini hakujibu. Alisema: Je, niswali au nimjibu mama? Mamake akaja tena na akamwita, hakumuitikia. Mama alimuapiza kwa kukosa kumwitikia:

“Ewe Allah عَزَّوَجَلَّ mwepushe huyu na mauti hadi wakati ule ambapo atauona uso wa mwanamke mpotevu.”

Juraij alikuwa kwenye mahali pa ibada. Mwanamke mmoja akasema: nitamtongoza. Kwa hivyo alikuja na akaanza kumsemesha lakini Juraij akampuuza. Mwishowe alijipeleka na kujisalimisha kwa mchungaji. Matokeo yake ni kwamba alipata mtoto na akamuhusisha na Juraij. Watu walimwendea Juraij katika maskani yake ya ibada wakapavunja, wakamtusi na wakamfurusha.

Juraij alitawadha na akaswali na baadaye akamwendea mtoto na akamuuliza: Ewe mtoto! Baba yako ni nani? Akajibu: Mchungaji fulani. (Watu wakamwomba Juraiji msamaha) Baadaye wakajitolea kwa Juraij: Tutakujengea pahali pa ibada kwa kutumia dhahabu. Akasema: La, pajengeni jinsi palivyokuwa (kwa udongo). (*Sahih Bukhari, uk. 39, Juzuu. 2, Hadithi 2482; Sahih Muslim, uk. 1380, Hadith 2550*)

Rehema za Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ ziwashukie na tupate msamaha kwa baraka zao.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Kutembea Maili Sita Katika Mawe (Ya Moto) Ya Kutoa Malengelenge Huku Mama Akiwa Mabegani

Haki za wazazi ni nyingi, hatuwezi kuzitekeleza (kama inavyotakiwa). Mmoja katika maswahaba wa Mtume رَضِيَ اللَّهُ تَعَالَى عَنْهُ alisema katika hadhira iliyobarikiwa ya mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ: Kulikuwa na mawe ya moto sana njiani kiasi ya kwamba endapo kipande cha nyama mbichi kingewekwa juu yake kingeiva na kuwa nyama choma!

Nilimbaba mamangu mgongoni nikatembea naye kwa maili sita. Je, mimi niko huru kutokana na utekelezaji wa haki za mama? Mtume صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akasema: Hilo linaweza kuwa ni fidia ya uchungu mmoja tu katika yale machungu ya uzazi aliyovumilia wakati akikuzaa.

Rehema za Mwenyezimungu عَزَّوَجَلَّ ziwashukie na tupate msamaha kwa baraka zao.

Ingekuaje kama mwanamume angekuwa ndiye mwenye kuzaa mtoto badala ya mwanamke!

Ndugu wapendwa waislamu! Bila ya shaka mama ndiye anayepata shida nyingi kutokana na mtoto wake. Ni mama pekee ndiye anayehisi na kujua uchungu wa uzazi.

A’la Hadrat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ anasema katika Fatwa Razaviyyah Sharif Juzuu 27 uk. 101: Mwanamume hupata starehe tu lakini mwanamke ndiye apataye shida kwa muda mrefu. Humbeba mtoto tumboni kwa miezi tisa na kupata shida katika kutembea, kuamka, kukaa chini na hukaribia kufa wakati wa kujifungua kutokana na uchungu wa uzazi. Kisha mwanamke ndiye ambaye huvumilia uchungu wa kuvuja damu baada ya kujifungua (nifasi) na huwa hawezi kulala kwa sababu ya machungu tofauti tofauti anayoyapata. Hiyo ndiyo sababu Allah عَزَّوَجَلَّ anasema:

حَمَلَتْهُ أُمُّهُ كُرْهًا وَوَضَعَتْهُ كُرْهًا وَحَمَلُهُ وَفِضْلُهُ ثَلَاثُونَ شَهْرًا ط

“Mamake alimbeba tumboni kwa shida, na akamzaa kwa shida na akambeba na kumnyonyesha kwa miezi thelathini.”

[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sura 26, Al-Ahqaf, aya 15)

Kwa hivyo kuzaliwa kwa kila mtoto ni miaka mitatu mfululizo ya uchungu mkali kwa mwanamke. Iwapo mwanamume ndiye angekuwa mwenye kuzaa hata kama ni mwana wa panya, hangejaribu tena maishani mwake. (*Fatawa Razaviyyah (Jadid) uk. 27, Juzuu 101*)

Mke Anastahili Kuhurumiwa

Ndugu wapendwa waislamu; kulingana na fatwa iliyobarikiwa ya A’la Hadarat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ hakuangazia umuhimu wa mama peke yake bali hata wa mke. Mume ni lazima awe na huruma zaidi kwa mkewe wakati akiwa mja mzito. Ni wajibu wake

kumsaidia katika kila jambo. Asimwachilie kufanya kazi yoyote ngumu. Asimtie katika taharuki kwa kumrukia kwa maneno au kwa njia yoyote ile. Kwani anastahili ampumzishe sana iwezekanavyo. Wakati wote anapopendezwa na mtoto wake, anastahili pia kumtizama mamake mtoto kwa jicho la huruma kwa yale mazito aliyohimili wakati wa kumzaa mtoto huyo kipenzi chake.

Maelezo Kuhusu Sheria Za Kunyonyesha Mtoto.

Aya ya Quran ambayo imetajwa katika fatwa iliyobarikiwa ya A'la Hadrat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ "Na kumnyonyesha kwake ni kwa miezi thelathini na hili limehusiana na uhusiano wa maziwa na kuharamishwa kwa Nikah. Imetajwa katika Bahar –e-Shariat, Juzuu 2 uk. 36 kilochochapishwa na Maktaba-tul-Madinah kwamba: Mtoto mchanga atanyonyeshwa kwa miaka miwili (kulingana na miaka ya Hijra). Hairuhusiwi zaidi ya hapo, awe mtoto ni wa kike au wa kiume. Hili ni jambo linalofanyika sana miongoni mwa watu fulani kumnyonyesha mtoto wa kike miaka miwili na wa kiume miaka miwili na nusu. Jambo hili ni makosa. Sheria hii (ya miaka 2) ni ya kunyonyesha pekee. Na kwa Nikah kuwa haramu, muda wake ni miaka miwili na nusu. Hili lina maana kwamba japokuwa kunyonyesha baada ya miaka miwili ni haram, lakini akinyonyesha kwa miaka miwili na nusu (kulingana na miaka ya Hijra) Hurmat-e-Nikah itathubutu. Na iwapo ataendelea kunyonyesha baada ya hapo,

kitendo hiki hakitathubutisha Hurmat-e-Nikah iwapokuwa kuendelea na jambo hili hakukubaliwi.

Ni Wajibu Kuwa Mtiifu Kwa Wazee Hata Wakiwa

Wabaya

Seyyiduna Abdullah bin Abbas رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا alisema kwamba Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: “Iwapo mmoja wenu asubuhi yake itampata akiwa mtiifu kwa wazazi wake ,milango miwili ya pepo huwa wazi kwake katika kipindi hicho cha subuhi na iwapo ni mzazi mmoja tu kati ya wazazi wake ambaye yuko hai basi ni mlango mmoja wa pepo unaofunguliwa. Na kwa yule ambaye jioni yake itampata akimkosea Allah عَزَّوَجَلَّ kwa ajili ya haki za wazazi, kwa yeye milango miwili ya moto huwa wazi kuanzia asubuhi na mlango mmoja tu kwa ambaye mzazi mmoja yuko hai. Mtu mmoja akauliza iwapo je, wazazi wake wanamtesa. Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akajibu: Hata kama wanakutesa, hata kama wanakutesa, hata kama wanakutesa: *(Shuab-ul-Iman, uk. 206, Juzuu 6, Hadithi 7916)*

Ndugu waislamu! Bila ya shaka mwenye kufurahisha wazazi wake amebahatika sana. Na yule mwenye kuwakasirisha wazazi wake hakuna kingine chochote (atakachokipata) ila maangamizi. Allah عَزَّوَجَلَّ anasema katika sura ya 15, Bani israil/ aya 23 hadi 25:

وَبِالْوَالِدَيْنِ إِحْسَانًا ۗ إِمَّا يَبْلُغَنَّ عِنْدَكَ الْكِبَرَ أَحَدُهُمَا أَوْ كِلَيْهِمَا فَلَا
تَقُلْ لَهُمَا آفٍ وَلَا تَنْهَرْهُمَا وَقُلْ لَهُمَا قَوْلًا كَرِيمًا ﴿٢٣﴾ وَأَخْفِضْ لَهُمَا
جَنَاحَ الدَّلِّ مِنَ الرَّحْمَةِ وَقُلْ رَبِّ ارْحَمْهُمَا كَمَا رَبَّيْنِي صَغِيرًا ﴿٢٤﴾
رَبُّكُمْ أَعْلَمُ بِمَا فِي نُفُوسِكُمْ ۗ

Na (ameagiza) kuwafanyia wema (mkubwa) wazazi. Kama mmoja wao akifikia uzee (naye yuko) pamoja nawe au wote wawili basi usiwaambie hata Ah! Wala usiwakemee na useme nao kwa msemu wa heshima (kabisa).

Na uwainamishie bawa la unyenyekevu kwa (njia ya kuwaonea) huruma (kwa kuwaona wamekuwa wazee). Na useme: “Mola wangu! Warehemu (wazee wangu) kama walivyonilea katika utoto wangu”. Mola wenu anajua sana yaliyo nyoyoni mwenu.

[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sura 26, Bani israil, aya 15)

Mama Huvumilia Kinyesi Cha Watoto Wake Wakiwa Wachanga

Ndugu waislamu wapendwa! Kutokana na aya iliyotajwa hapo juu, Allah عَزَّوَجَلَّ ametuamrisha kuwahurumia wazazi hususan amehimiza kuwashughulikia wakiwa wakongwe. Umri wa ukongwe wa wazee unamtia mtu katika mtihani. Wakati mwingine wakiwa wakongwe wazee huwenda haja kubwa kitandani na

watoto wao hukasirika. Lakini litiye hilo akilini! Kuwahudumia wazazi katika hali hiyo ni lazima!

Mama pia alishika kinyesi cha mwanawe alipokuwa mchanga. Kutokana na uzee na magonjwa mbalimbali, na hata kama wamekuwa wasumbufu, dhaifu, wanalalamika kwa mambo yasiyo na maana, wanapigana, wanayafanya maisha yako yawe na tabu lazima uwe na subira; subiri na uwaheshimu. Sahau kabisa kuwakosea wazee, au kuwarukia na hutakiwi hata kusema ‘Ah!’ kwao au utakuwa katika hasara na kuangamia duniani na akhera kwa sababu mwenye kuwakasirisha wazazi wake hupata mateso na laana katika dunia na pia hustahili kupata adhabu ya moto kesho akhera. Acha kuwaudhi wazee la sivyo utakuwa katika hasara kubwa.

Dil dukhana chor dayn Man Bap ka

Warnah is mayn hay khasarah ap ka

(Wasail-e-Bakhshish, uk. 377)

Maiti Iliyofanana Na Punda

Sayyiduna Awwam bin Hawshab رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ (ambaye alikuwa mmoja wa Tabii Tabiin na alifariki mwaka 148 Hijri) alisema: Wakati mmoja nilipita karibu na makaburi ambayo yalikuwa nje ya kijiji. Baada ya swala ya Asr, kaburi moja lilifunguka na akatoka mtu mmoja aliyekuwa na sura ya punda na mwili wake ukiwa na umbo la binadamu. Alilia mara tatu kama punda na baadaye akarudi kaburini na kaburi likafungika.

Mama mmoja mzee alikuwa akishona pamba. Mwanamke mwingine akanambia: Unamwona yule mama mzee? Niliuliza: Kwani ana nini? Akasema (Yule mwanamke) Yule mama mzee ni mamake yule aliyekaburini. Alikuwa mlevi; siku zote aliporudi nyumbani baada ya kulewa saa za jioni, mama yake alikuwa akimshauri: Ewe mwanangu, muogope Allah عَزَّوَجَلَّ. Lini utaacha kulewa! Alikuwa akimjibu kwa kusema: Unalia kama punda. Mtu yule alifariki baada ya swala ya Asr. Kutoka siku aliyofariki, kila siku baada ya swala ya Asr kaburi lake hufunguka na yeye hutoka akilia kama punda mara tatu na baadaye hurudi kaburini na kaburi hujifunga. *(At- Targhib-wat-Tarhib, uk. 226, Juzuu. 2 Hadith 17)*

Maombi Ya Mwenye Kuwaasi Wazazi Wake

Hayakubaliki

Ndugu wapendwa waislamu, tutubie mbele ya Allah عَزَّوَجَلَّ mwingi wa rehema na msamehevu na tumwombe usalama.

Ah! Kuwaudhi wazazi wako ni hasara kubwa na matokeo yake ni mateso makubwa. Imeelezwa katika hadith kwamba:

عَذَابُ الْقَبْرِ حَقٌّ Mateso ya kaburini ni ukweli. *(Sunan Annasaai uk 225 Hadithi 1305)*. Wakati mwengine dalili zake zinaonyeshwa hapa duniani ili watu wapate kujifunza.

A'la Hadrat رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema katika kujibu moja ya maswali aliyoulizwa kuhusu mwenye kumuasi babake kwamba: Mwenye kumkosea baba amemkosea Allah عَزَّوَجَلَّ na hasira za baba ni

hasira za Allah ﷻ. Iwapo mtu atawaridhisha wazazi wake, basi wao ndiwo pepo yake na iwapo atawaudhi basi wao ndiwo moto wake.

Hakuna swala yake ya faradhi, sunnah au vitendo vyake vizuri vitakavyokubaliwa mpaka amridhishe babake. Mbali na mateso ya akhera, mikosi mikubwa itamkumba hapa duniani na kuna hatari wakati anapokufa ﷻ hataweza kutamka shahada. ((*Sunan Annasaai*, uk 225, *Hadithi 1305*; *Fatawa Razawiyyah (Jadid)*, uk. 383-385, *Juzuu. 24*).

Allah ﷻ atuepushe (kwayo), hata kama wazazi ni makafiri (wasioamini Mungu) ni wajibu kuwa mpole kwao kwa mujibu wa sheria. Sadr-ush-Shariah, Badr-ut-Tariqah, Allamah Maulana mufti Muhammad Amjad Ali A'zami رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ aliandika kwa kumrejelea Alamgiri katika Bahar-e-Shariat Juzuu 2 uk. 452 kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah kwamba: Iwapo wazazi wa Muislamu ni makafiri na wamemtaka awapeleke kwenye hekalu la kuabudu masanamu, asifanye hivyo na iwapo watamtaka awaregeshe, basi awaregeshe. (*Fatawah Alamghiri*, uk. 350, *Juzuu. 6*)

Mwenye Kumtusi Mamake/Babake

Wale waliozoea kuwatusi kina mama wa wenzao ni watu waliofedheheka. Sadr-ush-Shariah' Badr-ut-Tariqah, Allahmah Maulana Mufti Muhammad Amjad, 'Ali A'zami رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ aliandika katika Bahar-e-Shariat, Juzuu 16 uk. 195 kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah kwamba: Mtume

صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: Ni katika madhambi makubwa kwa mtu kuwatusi wazazi wake. Watu waliuliza: Ewe Mtume wa Mwenyezimungu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ je! Kuna yeyote ambaye huwatusi wazazi wake? Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akajibu: Ndiyo. Ni wakati ule anapomtusi baba wa mtu mwengine ndiyo kama ambaye anamtusi babake na anapomtusi mama wa mtu mwengine ni kama ambaye anamtusi mamake. Baada ya kusimulia hadithi hii ‘Allamah Maulana Mufti Muhammed Amjad ‘Ali A’zami رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ anasema: maswahaba watukufu عَلَيْهِمُ الرِّضْوَانُ pamoja na kuwa walishuhudia wakati wa ujahiliya hawakuelewa ni kwa nini mtu awatusi wazazi wake (kweli mtu anaweza kuwatusi wazazi wake!) jambo hili (kwao) haliwezekani! Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ akafafanua kwamba ni kule wazazi kutusiwa na wengine. Na sasa umefika wakati baadhi ya watu wanawatusi wazazi wao wenyewe na wala hawawathamini kabisa.

(Bahar-e-Shariat)

Wale Wenye Kuning’inia Na Matawi Ya Moto

Seyyidina Imam Ahmad bin Hajr Makki Shafi’i رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ anasimulia: Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: Katika usiku wa Miraj (safari ya mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kwenda mbinguni) niliwaona baadhi ya watu wakining’nia na matawi ya moto.

Basi nikauliza: Ewe Jibril, الَّذِينَ يَشْتُمُونَ آبَاءَهُمْ وَأُمَّهَاتِهِمْ فِي الدُّنْيَا hawa ni watu gani? Akajibu: Hawa ni watu ambao walikuwa wakiwatusi mama zao na baba zao ulimwenguni. *(Azzawajir*

‘Aniqtiraf-il-Kabair, uk. 139, Juzuu 2)

Makaa Mengi Ya Moto Kama Matone Ya Mvua

Inasemekana kwamba: Mwenye kuwatusi wazazi wake, kaburi lake huangukiwa na makaa mengi ya moto kama vile matone ya mvua yanavyoanguka ardhini kutoka angani. (*Azzawajir 'Aniqtiraf-il-Kabair, uk.140, Juzuu 2*)

Kaburi Lavunja Mbavu

Imesimuliwa ya kwamba: Wakati mwili wa mtu aliyekosa kutii wazazi wake unapozikwa, kaburi humbana sana mpaka mbavu zake zikashikana (baada yakuvunjwa). (*Azzawajir 'Aniqtiraf-il-Kabair, uk. 140, Juzuu 2*)

Hataingia Peponi

Imeelezwa na Sayyiduna 'Abdullah bin Umar رَضِيَ اللهُ تَعَالَى عَنْهُمَا kwamba mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema watu watatu hawataingia peponi:

1. Mwenye kukosa kuwatii wazazi wake.
2. Dayuthi. (mtu asiyemuonea mkewe wivu)
3. Mwanamke mwenye kujifananisha na mwanaume.
(*Al-Mustadrak uk.525, Juzuu Hadithi 252*)

Endapo Baba Na Mama Wanateta, Watoto Wafanye Nini?

A'la Hadrat رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ anasema: Endapo kutatokea utesi kati ya baba na mama basi watoto wasimuunge au kumsaidia yeyote kati yao. Hawatakiwi kuwa wakali kwa baba yao kwa sababu ya mapenzi ya mama yao. Kumuudhi baba yako, kumjibu kijeuri au kuzungumza naye kisuluhivu kwa kumtazama machoni ni haramu. Na huku nikumkosea Allah عَزَّوَجَلَّ Haifai watoto kusaidia upande wowote kati ya baba na mama katika hali kama hiyo (ya kuteta). Wote wawili ni pepo yao na moto wao. Yeyote atakayemuudhi mmoja kati yao, basi atakuwa ni mwenye kustahili (adhabu ya) moto.

Mtu haifai kumtii yeyote na kusababisha kumuasi Allah عَزَّوَجَلَّ. Kwa mfano iwapo mama atamtaka mtoto wake amuudhi babake kwa njia yoyote basi mtoto asikubali kufanya hivyo. Na kwa sababu hii mamake akikasirike, amuache. Vile vile iwapo baba atamtaka amuudhi mama, asifanye.

Wanavyuoni wamegawanya haki kati ya baba na mama. Ikiwa ni katika mas'ala ya huduma mama amepewa kipao mbele na ikiwa ni katika mas'ala ya kuheshimu, baba amewekwa mbele kwa sababu baba wa mtu ndiye kiongozi wa mama pia. (*Fatawa Razawiyyah (Jadid), uk. 399, Juzuu 24*)

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Endapo Wazazi Watawaamrisha Kunyoya Ndevu

Basi Musiwafuate

Tumekuja kujua kuwa endapo wazazi watakuamrisha kufanya jambo ambalo ni kinyume na sheria (haram), basi usiwatii. Kuwatii (katika kufanya mambo ambayo ni kinyume na sheria) ni dhambi. Kwa mfano wakikwambia kusema uwongo au kunyoya ndevu, au kuzipunguza ziwe kidogo zisijae mkononi basi usiwakubalie kabisa kwa mambo haya hata kama wataudhika kiasi gani. Na iwapo utawakubalia (katika mambo ya haram), bila ya shaka utakuwa ni mwenye kumkosea na kumuasi Allah **عَزَّوَجَلَّ** Vile vile ikiwa mama na baba wametalikiana, na mama akakulazimisha usikutane na babako, basi amri kama hii haifai kufuatwa. Itakubidi ukutane na babako na umuhudumie. Japokuwa wametengana, uhusiano (wao) na watoto haujakatika. Watoto wanastahili kutekeleza haki sawa kati ya wazazi wote wawili.

Ni Kipi Mtu Anastahili Kufanya Endapo Wazazi

Wake Watakufa Wakiwa Hawana Radhi Naye?

Iwapo wazazi wa mtu watakufa wakiwa hawana radhi naye basi anastahili kuwaombea maghfira sana kwani zawadi kubwa kwa maiti ni kuwaombea maghfira na awapelekee thawabu nyingi. Inatarajiwa kwamba wazazi wake wawili waliofariki huenda wakaridhika naye iwapo atawapelekea kwa mfululizo zawadi ya matendo mema.

Imetajwa katika Bahar-e-Shariat' Juzuu 16 uk 197 kilochochapishwa na Maktaba-tul-Madinah kwamba: Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: Wazazi wa mtu au mmoja wao akifariki katika hali ambayo alikuwa amewakosea, basi awaombe msamaha kwa kiasi ya kwamba Allah عَزَّوَجَلَّ ataliandika jina lake miongoni mwa watu wema. (*Shuab-ul-Imam, uk. 202, Juzuu 6, Hadith 7902*)

Ikiwa inawezekana, nunua vijitabu na vitabu vingi uwezavyo kutoka kwa Maktabatul-Madinah na usambaze kwa ajili ya Isal-e-Sawab (thawabu ziwafikie wazazi waliokufa). Iwapo utataka jina la mzazi wako au anwani yako iandikwe katika vitabu na vijitabu hivyo basi wasiliana na Maktaba-tul-Madinah.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Kulipia Wazazi Madeni

Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: Mwenye kutekeleza dhima ya wazazi wake baada ya wao kufa na kuwalipia madeni na asiwatakanishe kwa kuwatusi wazazi (wa watu) wengine, atakuwa ni mwenye kuandikwa kuwa miongoni mwa wale ambao waliowatendea wazazi wao mema hata kama alikuwa hawatii (wakati wa uhai wao) na yule ambaye hataitekeleza dhima ya wazazi wala kuwalipia madeni yao na kuwafanya watukanwe kwa sababu ya (yeye) kuwatusi wazazi (wa watu) wengine, ataandikwa miongoni mwa wale waliokosa kutii

wazazi wao hata kama alikuwa akiwatendea mema wakati wa uhai wao. (*Al-Mu'jam Awsat, uk. 232 Juzuu 4, Hadith 5819*)

Faida Ya Kuzuru Kaburi La Wazazi Siku Ya Ijumaa

Mtume kipenzi صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alisema: Mwenye kuzuru makaburi yote mawili ya wazazi wake au mmoja wao kila siku ya Ijumaa, Allah عَزَّوَجَلَّ atamsamehe dhambi zake na ataandikwa katika wale wenye kuwatendea mema wazazi wawili. (*Jami' Tirmizi uk. 97, Hadith 130*)

Idhaa Ya Madani Italeta Mabadiliko Ya Madani

Katika Kila Nyumba

Ndugu waislamu wapendwa! Ili kuepuka kuwaasi wazazi na kuwa na hamu ya kuwa watiifu, ni nyoyo zenu kumpenda Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ na kuzifanya ziwe ni shina la mapenzi ya Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ. (Basi) Shikamaneni na mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islam إِنَّ شَاءَ اللهُ عَزَّوَجَلَّ. Kwa baraka ya mazingira haya ya Madani, tutapata fursa ya kutekeleza sunnah, matendo mazuri, kujiepusha na madhambi na kuhifadhi imani zetu.

Kwa kujifunza Sunnah, fanya mazoea ya kusafiri siku tatu na Madani Qafilah pamoja na wapenzi wa Mtume صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kila mwezi. Tumieni mchana na usiku (kufanya ibada) kwa mujibu wa 'Madani In'amat' iliyotolewa na Madani Markaz na

ufanye Fikr-e-Madinah angalau kwa dakika 12 na ujaze kadi yako ya Madani In'amat. **إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ** Utakuwa ni mwenye kufuzu katika dunia hii na kesho akhera. Ili (upate) kuelewa faida ya mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami, (sasa) soma baraka ya Madani.

Muhtasari wa tukio lililoelezwa na Muballigh-e-Dawat-e-Islami kutoka Mirpur 11 (Dhaka, Bangladesh) ni kwamba wakati mmoja nilikutana na mtu nilipokuwa nikienda pahali fulani. Aliponiona akasema: Unajua pale ninapoenda pamoja na mke wangu na watoto? Baadaye akajijibu mwenyewe: Hakika mimi na wazazi wangu tulikuwa na uhasama kati yetu. Kutokana na maadili niliyoyapata kwa kuangalia Bayan 'Man Bap ke Huquq (Haki za Wazazi) katika idhaa ya Madani, nimefahamu kwamba nimefanya kosa kubwa sana kwa kutowatii wazazi. Kwa hivyo naenda kwa wazazi wangu pamoja na mke wangu na watoto kuwabembemebeza ili wanisamehe. Ewe Allah **عَزَّوَجَلَّ** ipe mafanikio makubwa Dawat-e-Islami na Idhaa ya Madani.

آمِينَ بِجَاهِ النَّبِيِّ الْأَمِينِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Alikatwa Mguu Kwasababu Ya Maapizo Ya Mama

Ndugu wapenzi waislamu! Kutokana na Madani Bahar, tumepata kufahamu faida za Idhaa ya Madani. Vile vile katika Madani Bahar kumeelezwa ‘Haki za Wazazi’ kwa uwazi. Kwa hakika ni vigumu mno kutekeleza kwa ukamilifu haki za wazazi. Mtu anawajibika kutekeleza haki za wazazi katika umri wake wote na ajiepushe na kuwaudhi wazazi wake. Wale watu ambao huwaudhi wazazi wao, hata duniani, huona matokeo mabaya.

Shaykh ‘Allamah Kamaluddin Damari رَحْمَةُ اللهِ تَعَالَى عَلَيْهِ anasimulia kwamba Zamakhshari (ambaye alikuwa mwanachuoni mkuu wa kundi la Mu’tazilah) alikatwa mguu wake mmoja. Watu walipouliza sababu yake, alielezea: Jambo hili lilitokana na maapizo ya mamangu. Tukio hili lilitokea nikiwa mdogo. Nilimshika ndege na nikamfunga uzi kwenye mguu wake. Alibahatika akaruka kutoka mkononi mwangu na akaingia kwenye ufa wa ukuta lakini ule uzi ulikuwa nje unaning’inia. Niliuvuta ule uzi kwa nguvu sana. Yule ndege akatoka kwa kifafa (kama aliyeshikwa na kifafa) akiwa na maumivu makali. Maskini mguu wake ulikuwa umekatwa na uzi. Mamangu alikiona kitendo hiki cha uchungu na hakuweza kuvumilia. Kutokana na hasira akaniapiza: Namuomba Allah عَزَّوَجَلَّ akukate mguu wako kama vile ulivyomfanya huyu ndege asiye na hatia.

Na ikafanyika hivyo. Baada ya muda fulani nilisafiri kwenda Bukhara kujifunza elimu ya dini na nikaanguka nilipokuwa juu ya kipando na mguu wangu ukaumia vibaya. Nilipofika Bukhara,

nilipata matibabu mengi lakini mguu haukupona. Baadaye ilibidi ukatwe. (kwa hivyo apizo la mamangu likatimia). (*Hayat-ul-Haywan-ul-Kubra, uk. 163, Juzuu 2*)

Omba Msamaha Kwa Wazazi Kwa Kuwaangukia Miguuni

Ndugu wapenzi waislamu! Iwapo wazazi wako ama mmoja wao ana hasira, bila ya kuchelewa zaidi, omba msamaha kwa kulia, kwa kuunganisha mikono yako mbele yao na kuwaangukia miguuni mwao. Tekeleza matakwa yao ya halali kwa sababu kufaulu hapa duniani na kesho akhera kunategemea jambo hili. Kwa maelezo zaidi kuhusu haki za wazazi, tafadhali angalia kaseti (kanda) hizi mbili za video.

1. ‘Man Bapko Huquq’ (Haki za wazazi).
2. Kaseti (kanda) ya video ya Madani Muzakarah ilifanyika wakati wa I’tikaf ya Ramadhan-ul-Mubarak (1430 Hijri) iitwayo ‘Walidain kay na-Farmanon ka Anjam’ (Malipo ya kuwaasi wazazi) ilionyeshwa na Maktaba-tul-Madinah.

Acha kuuudhi moyo wa wazazi wako

Ama utakuwa katika hasara kubwa

Takasa moyo wako kutokana na vitimbi vya waislamu.

Fuata nyayo za Mtume kipenzi cha Allah

Ewe Allah, ombi la Attar ni kwamba kila mtu ashikilie sunnah za Mtume (صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ) Ndugu wapenzi waislamu! Kwa

kumalizia Bayan mpaka mwisho, nitakuwa na fursa ya kuwatajia baraka za Sunnah ya Mtume na baadhi ya Sunnah na adabu za kiislamu. Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ amesema: Mwenye kupenda Sunnah zangu ananipenda mimi na anayenipenda mimi atakuwa pamoja nami peponi.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Sunnah Na Adabu Za Kutembea (15)

1. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika sura ya 15, Sura Bani Israil, aya ya 37, iliyotafsiriwa na Kanz-ul-Iman Sharif:

وَلَا تَمْشِ فِي الْأَرْضِ مَرَحًا

إِنَّكَ لَنْ تَخْرِقَ الْأَرْضَ وَلَنْ تَبْلُغَ الْجِبَالَ طُولًا ﴿٣٧﴾

“Na wala msitembee kwa maringo juu ya ardhi; hamuwezi kuipasua ardhi na wala kufikia (urefu wa) kilele cha milima.

2. Maneno ya kupendeza ya Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ yameelezwa katika Bahar-e-Shariat, Juzuu ya 16 uk. 78 iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah kwamba: Mtu mmoja aliona fahari kutembea kwa kibri kwa kuwa amejifunika kwa vitambara viwili vya nguo. Ardhi ikamvuta ndani yake (kummeza) na itaendelea kumvuta hadi Siku ya Hukumu (Kiyama). (*Sahih Muslim, uk. 5465*)

3. Wakati mwengine Mtume mpendwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa akitembea huku ameshikilia mkono wa swahaba wake kwa mkono wake uliobarikiwa. (*Al-Mu'jam Kabir, uk. 162, Juzuu 7*). (Lakini) Mtu hafai kushikilia mkono wa Amrad (mvulana anayevutia). Kwa kuushikilia mkono wake au kupeana mikono au kumkumbatiana kwa tamaa ni haramu na ni kitendo ambacho kinaweza kumpeleka mtu motoni.
4. Wakati Mtume mtukufu صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alipokuwa akitembea, alikuwa صَلَّى اللهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ kidogo akiinama mbele kama ambaye anateremka mlima. (*Shamail-e-Tirmizi, uk. 87, Hadith 118*)
5. Usitembee kwa kibri kabisa, usivae dhahabu, au mkufu wowote uliotengenezwa kwa chuma na usiache vifungo vyako (vya shati) vya mbele wazi ili kujionyesha. Huu ni mtindo wa watu wasiokuwa na busara, wenye kibri na wenye kutenda dhambi. Ni haramu kwa mwanamume kuvaa dhahabu shingoni na kuvaa aina nyingine za mikufu ya chuma.
6. Iwapo hakuna viziwi, tembea pembeni mwa barabara kwa hatua za wastani. Usiwe na haraka sana kiasi ya kwamba watu waanze kukuangalia (na kuulizana) unaenda wapi kwa haraka namna hiyo na usitembee polepole sana kiasi ya kwamba mwenye kukuona anaweza kudhania kuwa wewe ni mgonjwa.

7. Si katika Sunnah kuangalia huku na kule (bila ya sababu) wakati unatembea. Tembea kwa heshima na macho yako yakiangalia chini. Sayyiduna Hassan bin Abi Sinan عَلَيْهِ رَحْمَةُ الرَّحْمَانِ alikwenda kwa swala ya Iddi. Wakati yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ aliporudi nyumbani, mkewe akamuuliza: Umewaona wanawake wangapi? Yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ akanyamaza. Wakati mkewe alipomtiriri sana, yeye رَحْمَةُ اللَّهِ تَعَالَى عَلَيْهِ alisema: ‘Niliendelea kutazama vidole vya miguu yangu tokea nilipotoka hadi niliporudi kwako.’ (*Kitab-ul-Wara’ ma’ Mawsu’ah Imam Ibin Abi Dunya, uk. 205, Juzuu 1*)

سُبْحَانَ اللَّهِ عَزَّوَجَلَّ Watu wanaomuogopa Allah hawaangalii huku na kule bila ya sababu wakiwa wanatembea, hususan kukiwa na watu wengi kwani wanaweza kumwangalia mtu wasiyeruhusiwa kumwangalia kwa mujibu wa sheria! Huu ndiwo ucha Mungu! Sheria ni kwamba iwapo umemwangalia mwanamke bila ya kukusudia na ukaondosha macho yako kwa haraka basi hutakuwa umetenda dhambi.

8. Ni makosa kuangalia roshani ya mtu au kuchungulia madirishani bila ya sababu ya kimsingi.
9. Wakati unapotembea au kuteremka ngazi, hakikisha viatu vyako havifanyi kelele. Mtume wetu mpendwa صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَيْهِ وَآلِهِ وَسَلَّمَ alikuwa hapendi mlio wa viatu.

10. Iwapo kuna wanawake wawili waliosimama au wanaenda kwa shughuli zao, usiwapite katikati. Hadithi iliyobarikiwa yatukataza kufanya hivyo.
11. Si desturi kutema mate, kusafisha pua, kutia vidole vyako katika pua, kuchokora masikio, kutoa uchafu nguoni mwako kwa vidole, kujikuna sehemu zako za siri nakadhalika wakati unatembea, umekaa au umesimama mbele ya watu.
12. Watu wengine wana tabia ya kupiga mateke chochote kilichoko mbele yao. Hii ni tabia mbaya. Kuna hatari ya kuumia mguu wako pia. La ziada ni kwamba kupiga mateke magazeti au maboksi, pakiti na chupa tupu za maji zenye maandishi ni ukosefu wa heshima pia.
13. Unapotembea, fuata kanuni ambazo haziendi kinyume na Sheria. Kwa mfano, unapovuka barabara, jaribu kuvuka panapostahili kama vile kwenye alama za pundamilia au juu ya daraja.
14. Vuka barabara baada ya kuangalia upande wa trafiki (magari yanapotokea). Ukiwa katikati mwa barabara na gari linakaribia ni salama kusimama kuliko kukimbia la ziada ni kwamba kuvuka njia ya reli ambapo magari ya moshi hupitia ni kama kukaribisha kifo. Wale wanaofikiria magari ya moshi huenda polepole wakumbuke kwamba kuna uwezekano wa kutegeka na nyaya katika hali ya haraka na

baadaye kuanguka na kukanyagwa na gari moshi. Na kuna sehemu nyengine ambapo kupitia kwenye magari moshi ni kinyume cha sheria. Zingatia sheria hizi, hususani kwenye vituo vya magari.

15. Tembea kwa dakika 15 ukifanya dhikr na umswalie Mtume kila siku ukiwa na na niya ya kupata nguvu za kufanyia ibada. *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ* utabakia na afya. Njia bora ya kutembea ni kule kwenda kwa hatua za haraka kwa dakika 15 za mwanzo, mwendo wa wastani kwa dakika 15 zinazofuatia na tembea kwa hatua za haraka kwa dakika 15 za mwisho. Ukifuata mtindo huu, kiwiliwili chote kitapata mazoezi. *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ* mfumo wa mmeng'enyoye wa chakula utakuwa sawa *إِنْ شَاءَ اللَّهُ عَزَّوَجَلَّ*. Utanusurika kutokana na maradhi ya moyo na magonjwa mengine mengi.

Ukitaka Kujifunza Maelfu Ya Sunnah (Nyingi), Nunua Na Usome Vitabu Viwili,

1. Bahar-e-Shariat, Juzuu 16 na,
2. 'Suunatayn au Adab' (kilochapishwa na Maktabtul-Madinah).

Njia nyingine kubwa ya kujifunza Sunnah ni kusafiri na wapenzi wa Mtume katika Madani Qafilah ya Dawat-e-Islami.

صَلُّوا عَلَى الْحَبِيبِ صَلَّى اللَّهُ تَعَالَى عَلَى مُحَمَّدٍ

Orodha Ya Yaliyomo

KUBA BAHARINI 1

Aliyemsalia Mtume ﷺ Kwa Sauti Alisamehewa	1
Rehma Za Mwenyezimungu Ziwashukie Na Tupate Msamaha Kwa Baraka Zao.	4
Kidole Kilichoumia	4
Busu Kizingiti Cha Mlango Wa Pepo Kila Siku.	5
Aliwaacha Huru Watumwa Wawili Kwa Sababu Ya Kunyanyua Sauti Mbele Ya Mama	5
Pata Thawabu Ya Hijja Yenye Kutakabaliwa.....	6
Rafiki Wa Peponi	7
Rehma Za Mwenyezimungu ﷺ Ziwashukie Na Tupate Msamaha Kwa Baraka Zao.	8
Mtu Mmoja Anakuwa Bubu Kwa Kukosa Kumuitikia Mamake	9
Ni Bora Wazazi Kujizuiia Kuapiza (Watoto).....	9
Itabidi Kuregea Hata Kama Uko Ng'ambo.	9
Mtoto Mchanga Aongea!	10
Kutembea Maili Sita Katika Mawe (Ya Moto) Ya Kutoa Malengenge Huku Mama Akiwa Mabegani.....	12
Mke Anastahili Kuhurumiwa.....	13
Maelezo Kuhusu Sheria Za Kunyonyesha Mtoto.....	14
Ni Wajibu Kuwa Mtiifu Kwa Wazee Hata Wakiwa Wabaya.....	15

Mama Huvumilia Kinyesi Cha Watoto Wake Wakiwa Wachanga	16
Maiti Iliyofanana Na Punda	17
Maombi Ya Mwenye Kuwaasi Wazazi Wake Hayakubaliki	18
Mwenye Kumtusi Mamake/Babake	19
Wale Wenye Kuning'inia Na Matawi Ya Moto.....	20
Makaa Mengi Ya Moto Kama Matone Ya Mvua.....	21
Kaburi Lavunja Mbavu.....	21
Hataingia Peponi.....	21
Endapo Baba Na Mama Wanateta, Watoto Wafanye Nini?	22
Endapo Wazazi Watawaamrisha Kunyoya Ndevu.....	23
Basi Musiwafuate.....	23
Ni Kipi Mtu Anastahili Kufanya Endapo Wazazi Wake	
Watakufa Wakiwa Hawana Radhi Naye?	23
Kulipia Wazazi Madeni	24
Faida Ya Kuzuru Kaburi La Wazazi Siku Ya Ijumaa.....	25
Idhaa Ya Madani Italeta Mabadiliko Ya Madani Katika	
Kila Nyumba.....	25
Alikatwa Mguu Kwasababu Ya Maapizo Ya Mama	27
Omba Msamaha Kwa Wazazi Kwa Kuwaangukia Miguuni.....	28
Sunnah Na Adabu Za Kutembea (15).....	29

BARAKA ZA SUNNAH

Alhamdu Lillah ﷻ Sunnah za Bwana Mtume ﷺ zinafunzwa na kusomwa katika mazingira ya Madani ya **Dawat-e-Islami**, shirika la harakati za Qur'an na Sunnah la kimataifa lisilo jihusisha na siasa. Ijtimai ya kila wiki ya Karachi (Pakistan) huweko kila Alhamisi baada ya Swalatul-Maghrib huko Faizan-e-Madina, Mahalla Sodagaran, Old Sabzi Mandi.

Madani inakuomba ushiriki katika Ijtimai hii na ukeshe kwenye Faizan-e-Madina.

Jitahidi utoke na kundi la Wapenzi wa Bwana Mtume ﷺ katika **Madani Qafila** na huku ukileta **Fikr-e-Madinah** ujaze kadi yako ya **Madani In'aamaat** kila siku na umpe zimadaar (mwakilishi) wa eneo lako mnamo siku kumi za mwanzo za mwezi wa kiislamu. In'shaa-Allah ﷻ, kwa baraka ya kufuata utaratibu huu, tutaanza kushikamana na Sunnah za Mtume ﷺ. Tuta-chukia maasi na **tutailinda Imaani yetu**. Kila ndugu muislamu aweke niya **kuwa nitajaribu kurekebisha nafsi yangu na ya watu wa dunia nzima** In'sha-Allah ﷻ.

Kurekebisha nafsi zetu tutajaza **Madani In'aamaat**, na kurekebisha watu wa dunia nzima tutasafiri na **Madani Qafila**- In'sha-Allah ﷻ.

مكتبة المدينة

MAKTABA-TUL-MADINAH

Faizan-e-Madinah, Mahallah Saudagaran,
Old Sabzi Mandi, Karachi, Pakistan. P/c +92(21) 4921389-93-4126999
Email: maktaba@dawateislami.net Web: www.dawateislami.net